# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**


**Mkuu wa Shule 0752973027**

**M/Mkuu wa Shule: 0621294401**

**Mtaaluma :0762172880**

**Mhasibu: 0768312277**

**Matron: 0718900931**

**Mwalimu wa Nidhamu: 0766779822**

**Shule ya Sekondari Nsimbo**

**S.L.P. 304, MPANDA**


**Tarehe………………………..**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NSIMBO HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO MKOA WA KATAVI MWAKA……………………………**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka……………….na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Nsimbo ipo umbali wa Kilometa 14 Mashariki mwa Mji wa Mpanda Usafiri wa bajaji na pikipiki kutoka mjini Mpanda unapatikana katika kituo cha mabasi Mizengo Pinda Nauli ni Shilingi 6,000/= kwa pikipiki na Shilingi 5,000/= kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe……………., hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni tarehe……………….Mwisho wa kuripoti ni tarehe……………...

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia: -**

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi mbili za darasani rangi ya “light blue and yellow checked with black stripes masaai shuka” na Mshono ni linda box kubwa mbele na nyuma na malinda madogo mawili mawili pembeni na iwe ndefu hadi kwenye kifundo cha miguu **(zingatia maelekezo kuepuka usumbufu wa kushona sketi mara mbili)** rangi kama inavyoonekana hapa chini.



**NB:** Kama utapata changamoto ya upatikanaji wa kitambaa hicho na mshono unaweza kupata mafundi walio Jirani na Shule.

ii. Mashati mawili rangi nyeupe (aina ya halua) yenye kola, mikono mirefu ya darasani

iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe kwa darasani ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama (aina ya halua).

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya Ngozi vya kufunga na kamba vyenye shingo fupi na visigino vifupi.

v. Soksi jozi mbili nyeupe za shule.

vi. Sweta moja rangi ya blue ya kifalme (royal blue).

vii. Sare ya Michezo ni bukta na fulana(t-shirt) ya rangi ya pink iliyokolea, pia awe na raba jozi moja rangi nyeusi atakayoivaa kipindi cha michezo tu.




viii. Nguo za kushindia skirt mbili za rangi ya ugolo na Mshono ni linda box kubwa mbele na nyuma na malinda madogo mawili mawili pembeni na iwe ndefu hadi kwenye kifundo cha miguu **(zingatia maelekezo kuepuka usumbufu wa kushona sketi mara mbili).**



ix. Truck suit moja Kijani jeshi iliyokolea.

**NB:** Kama utapata changamopto ya upatikanaji wa kitambaa hicho na mshono unaweza kupata mafundi walio Jirani na shule.

i. Rangi ya Hijab la kushindia ni **ugolo** na ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama (aina ya halua).
ii. Tisheti mbili za rangi ya **LIGHT BLUE** iliyokorea zenye kola ya michirizi myeupe.

**2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo kulingana na mazingira ya shule yetu: -**

i. Madaftari 13 (kumi na tatu) quire four.
ii. **Ream (A4)** ya karatasi Mbili (2) (**aina ya double A**) kwa mwaka. iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
iii. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
iv. Scientific Calculator orijino yenye sifa ya(**fx-991**) kwa masomo ya Economics, Basic Applied Mathematics, Advanced Mathematics, chemistry na geography (lazima).
v. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe na vipimo vya inchi 2.5 kwa 6 kulingana na vipimo vya vitanda vilivyopo shuleni. Aidha, shule haina magodoro ya kukodisha.
vi. Mashuka pink Jozi 2, foronya ya mto pink 1, chandarua nyeupe 1 na blanketi na sio vinginevyo.
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 3 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko.
x. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 (mgumu na laini) na mfagio wa chelewa.
xi. Tochi kwa tahadhari pale umeme unapokatika.
xii. Dawa ya kusafishia vyoo (sabuni) aina ya **DEXI** Lita 10 (kwa mwaka) aina **nyingine haitapokelewa.**
xiii. Mwanafunzi aje na kandambili aina ya umoja (**lazima**) na mafuta mgando ya kupaka na si vinginevyo.
xiv. Khanga pair moja na taulo moja.
xv. Faili moja la plastiki kwa ajili ya kutunzia taarifa za mwanafunzi.

**2.3. Michango mbalimbali**

**Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB:**

i. Malipo hayo juu yenye jumla ya kiasi cha sh**. 80,000/=** yawekwe kwenye akaunti ya Shule,

**61910022051 NSIMBO SEC SCHOOL FUND** Benki ya NMB.

ii. Mwanafunzi aje na bima ya afya ya Taifa (NHIF) kwaajili ya matibabu kama hana aje na pesa taaslimu za kitanzania 50,400/= kwa ajili ya kufunguliwa bima ya afya ya Taifa (NHIF) (**bima ya Afya ni ya lazima**).

## 1. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kushiriki kikamilifu masomo ya alfajiri na usiku (morning &evening Preparation).
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule muda wote;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
ix. Kutunza mali za shule.
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu huleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kusuka nywele, Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.
viii. Uvutaji wa sigara.
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa.
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba.
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xv. Kudharau Bendera ya Taifa.
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.


**2. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu (lazima uje nazo).

**3.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.


**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule**



**Jina la Mkuu wa Shule: <u>Restuta G. Msafiri</u>**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**



**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- Mkuu wa shule 0750 286 031
- Makamu mkuu wa shule: 0621 294 401
- Mtaaluma mwandamizi: 0762172880
- Matron: 0718 900 931
- Mwalimu wa Nidhamu: 0766779822

**TAALUMA**

Kwa sababu shule ina uhaba wa vitabu, ikiwezekana ni vizuri aje na vitabu vitakavyo msaidia kwa masomo husika

**A. VITABU VYA KEMIA**

1. By. Chand Conceptual Chemistry for Class XI and XII
2. By Tanzania Institute of Education Advanced Level Inorganic Chemistry, Organic, Physical and General Chemistry
3. Advanced Chemistry Review (2000) – (2021) Paper I & II
4. Advanced Chemistry (Michael Ramsdens).

**B. VITABU VYA BIOLOJIA**

1. Taylor At El (1999) Biological Science, Third Edition. Tong Printing Press Hong Kong
2. Genn And Tods (1999) Understanding Biology 4th Ed. Stanley Thomes Ltd UK.

**C. VITABU VYA PHYSICS:**

1. S. Chand – Conceptual Physics XI Na XI

**D. VITABU VYA GEOGRAPHY**

1. Pritchard J.M. (1979), Afrika A Study Geography for Advanced Students. London Longman.
2. Kamili, 2, Physical Geography for Africa. Dar Es Salaam Afroplus Industries.
3. Msabila D.T. Physical Geography. Dar Es Salaam, Nyambari Nyangwine Publishers.

**E. VITABU VYA ECONOMICS**

1. Ambilikile C.M (2010) Economics for Advanced Level (PartI&II)
2. Gupta S.L And Chaturved D.D (2003) Managerial Economics, Texts and Cases
3. Othieno Okoth (2005), Contemporary Economics
4. Mudida R (2003) Modern Economics 1st Ed. Nairobi Kenya

**F. VITABU VYA SOMO LA HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI (TIE)**

**G. VITABU VYA SOMO LA ACADEMIC COMMUNICATIONS (TIE)**

**H. VITABU VYA ADVANCED MATHEMATICS**

1. Conceptual Advanced Mathematics for Secondary School Form V & VI by Petro L. Mayombya.

**I. VITABU VYA ENGLISH LANGUAGE**

1. **Plays**. The government Inspector by Nikolai by Gogoi, A Taste of Heaven by Farouk Topan. An Enemy of the people by Henrick Ibsen.
2. **Novels and short stories**. Animal farm by George Orwell.Chasing the Leopard.Finding the Lion by Julie Wakeman-linn. The Opportunist Elite by Nyambari C.M.Nyangwine.The Horizon univeiled by Followers Mwaisela.
3. **Poetry**. Summons.Poems from Tanzania by Richard S. Mabala et al.Poets of Africa. Lament of the Silent & other poems by Jred Angira.
4. Advanced level English language one and two (TIE)
5. Literature analysis
6. Advanced Learners Oxford English Dictionary

## J. VITABU VYA KISWAHILI

1. **Riwaya**:Dunia uwanja wa fujo. Ua la faraja.Mirathi ya hatari na Wasifu wa Siti Binti Saad.
2. **Tamthiliya**:Mukwava wa Uhehe.Shujaa Mirambo na Usaliti mjini.
3. **Ushairi**:Fumbo linaloelea.Malenga wa ziwa kuu.Andamo,msafiri safarini na Wosia wa Baba.

**KIAMBATA 'A'**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO**

**SHULE YA SEKONDARI NSIMBO**

Kumbukumbu Namba:

HISTORIA YA WAZAZI NA MTOTO ALIYE CHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE HII

**A. WAZAZI/WALEZI**

1. Jina la Baba ...................................................................................................................

2. Jina la Mama

3. Kama Baba si hai jina la Mlezi .................................................................................

4. Kama Mama si hai jina la Mlezi ..............................................................................

5. Kazi/shughuli ya Mzazi/Mlezi ..................................................................................

6. Anwani ya Mzazi/Mlezi..............................................................................................

7. Uraia wa Wazazi - Baba ..........................................................
   - Mama ..........................................................
   - Mlezi ..........................................................

8. Wakati wa likizo Mtoto/Mwanafunzi unatakiwa uende wapi? ..........................................

9. Jina la mtu aendako ............................................... Uhusiano na Mtoto/Mwanafunzi..................

**B: MWANAFUNZI**

1. Jina la mwanafunzi ........................................................................................
2. Tahasusi aliyochaguliwa ..................................................................................
3. Tarehe ya kuzaliwa ..........................................................................................
4. Mahali alipozaliwa ...........................................................................................
5. Namba ya cheti cha kuzaliwa ...........................................................................
6. Uraia ...................................................................................................................
7. Namba za simu za mwanafunzi ........................................................................
8. Namba za simu ya Baba/Mlezi ..........................................................................

9. Namba za simu ya Mama/Mlezi ………………………………………………………………………

10. Namba za simu ya mtu wa karibu ………………………………………………………………..

| | |
|---|---|
| SAHIHI YA BABA/MAMA/MLEZI | TAREHE |
| ……………………………………… | …………………………… |
| SAHIHI YA MWANAFUNZI | TAREHE |
| ………………………………………. | ………………………………. |
| PICHA YA MZAZI/MLEZI | PICHA YA MWANAFUNZI |

**KIAMBATA 'B'**

**FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by medical officer in respect to all forms of entrants
Student's full name……………………………………….
Age ……………………….
Years…………
Sex………………….
Blood count (red and white) ………………………………………………………………………………………………..
Stool examination ……………………………………………………………………………………………..
Urine analysis ………………………………………………………………………………………………………
Syphilis and other venereal disease test ……………………………………………………………………………….
……………………………………………………………………………………………………………………
T.B test…………………………………………………………………………………………………..
Eye Test ……………………………………………………………………………………………………….
Ears ………………………………………………………………………………………………………………
Abdomen …………………………………………………………………………………………………………
Urine for plant test ……………………………………………………………………………………………
Test for pregnancy ……………………………………………………………………………………………

ADDITIONAL INFORMATION

Defects, impotent (e.g. arms, legs etc.) infections, chronic or family diseases etc.
……………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………… ………………. I certify that the named above is fit to pursue further studies in agricultural/domestic education station ………………………………………………………………………………………………………………….

Signature…………………. Date……………………… Designation……………………………….

**KIAMBATA 'C'**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO**

**SHULE YA SEKONDARI NSIMBO**

**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE**

Mimi mzazi/mlezi wa ………………………………………………………………………. nimesoma kwa makini maagizo yote ninatambua kuwa kuchaguliwa kwangu kuingia shule ya sekondari ni bahati na zawadi kubwa kwa kuwa wengi wamekosa nafasi si kwa kuwa wameshindwa ila kwa sababu ni chache.

Hivyo nakubali kujiunga na shule ya sekondari Nsimbo ya Wasichana. Nitatii na kufuata sheria na taratibu zote za shule. Nitajitahidi kufanya kazi/kusoma kwa juhudi na maarifa na nitajitahidi kushirikiana na wenzangu kweli daima.

Nitalinda hadhi/heshima ya shule ya Sekondari Nsimbo na nitashirikiana na wenzangu kujenga misingi na historia nzuri ya shule.

Tarehe ……………………… Sahihi ya mwanafunzi …………………………………………………….

Mimi…………………………………….. Mzazi/Mlezi ………………………………………….. Nimeshuhudia mtoto wangu ……………………………………………… akikubali kwa hiari kujiunga na shule hiyo ninaamini mtajitahidi kumfunza na kumlea vizuri. Mimi pia naahidi kushirikiana nanyi kikamilifu katika kumlea binti yangu naamini tutakuwa tunawasiliana.

Tarehe ………………………………….. Sahihi ya Mzazi/ Mlezi …………………………………………….

**BAADHI YA VIFAA VINAVYO PATIKANA KATIKA DUKA LA SHULE NA BEI ZAKE KAMA UTAPENDA KIVINUNULIA SHULENI.**

## 1. STATIONERY

| S/NO | VIFAA | BEI |
|---|---|---|
| 1. | REAM PAPER (A4) | TSH. 12,000/= |
| 2. | COUNTER BOOK QUIRE 2 | TSH. 2,500/= |
| 3. | COUNTER BOOK QUIRE 3 | TSH. 3,500/= |
| 4. | COUNTER BOOK QUIRE 4 | TSH. 4,500/= |
| 5. | SCIENTIFIC CALCULATOR (FX 991) | TSH. 35,000/= |
| 6. | DAFTARI ZA MSOMI | TSH. 1,000/= |
| 7. | PENI | TSH. 200/= |
| 8. | MKEBE (MATHEMATICAL SET) | TSHS. 2,500/= |

## 2. VIFAA VYA USAFI

| S/NO | VIFAA | BEI |
|---|---|---|
| 1. | JEMBE NA MPINI | TSH. 8,500/= |
| 2. | BRUSH NGUMU | TSH. 4,000/= |
| 3. | BRUSH LAINI (SOFT BROOM) | TSH. 4,000/= |
| 4. | SQUIZER | TSH. 4,000/= |
| 5. | KWANJA | TSH. 6,000/= |
| 6. | REKI | TSH. 8,000/= |
| 7. | NDOO NDOGO LITA 10 | TSH. 6,000/= |
| 8. | FAGIO ZA CHELEWA | TSH. 2,000/= |

## 3. NGUO

| S/NO | NGUO | BEI |
|---|---|---|
| 1. | SHATI AINA YA HALUA | TSH. 18,000/= |
| 2. | SHUKA NYEPESI YA PINKI | TSH. 12,000/= |
| 3. | NETI | TSH. 12,000/= |
| 4. | SWETA | TSH. 15,000 |
| 6. | TRACK SUIT | TSH. 25,000/= |
| 7. | T-SHIRT | TSH. 16,000/= |
| 8. | SKETI | TSH. 35,000/= |
| 9 | GODORO 4” (2.5ft x 6 ft) | TSH. 55,000/= |
| 10 | JEZI (FULANA NA BUKTA) | TSH. 22,000 /= |
| 11 | VITABU VYA MASOMO YOTE | - |